SHIRIKA LA RELI TANZANIA

Jarida la
# RELI NA MATUKIO

Toleo namba 36, Aprili 2024

Habari | Makala | Matukio | Elimu | Picha



# WAZIRI MKUU ASHUHUDIA MAJARIBIO YA KWANZA TRENI YA SGR DAR ES SALAAM - DODOMA

Na Mwandishi wetu.


Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Kassim Majaliwa ashuhudia majaribio ya kwanza ya treni ya kisasa kutoka Dar es Salaam - Dodoma Aprili 21, 2024.

Treni ya Kwanza ya majaribio ilibeba viongozi mbalimbali wa Serikali, viongozi wa Dini, wakuu wa Taasisi za Serikali ,wasanii pamoja na wanahabari ilisafiri kutoka Dar es Salaam kwenda makao makuu ya nchi Dodoma kwa ajili ya sala maalumu ya kuliombea Taifa kuelekea kilele cha miaka sitini (60) ya Muungano wa Tanganyika na Zanzibar.

Waziri Mkuu alisema kuwa Serikali itaendelea kushirikiana na viongozi wa Dini ili kuendelea kudumisha Amani ,Upendo na kujenga nchi.

Inaendelea Uk. 2

## BUNGE LAPITISHA TRILIONI 1.511 KUENDELEZA MRADI WA SGR NCHINI Uk. 3



Waziri wa Uchukuzi Mhe. Prof Makame Mbarawa akiwasilisha hotuba ya bajeti ya Wizara ya Uchukuzi kwa mwaka wa fedha 2024/25 katika Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania jijini Dodoma hivi karibuni 2024.

# WAZIRI MKUU ASHUHUDIA MAJARIBIO YA KWANZA TRENI YA SGR DAR ES SALAAM - DODOMA



Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Kassim Majaliwa akiagana na baadhi ya viongozi kabla ya treni ya kwanza ya majaribio kuanza safari kuelekea jijini Dodoma, katika stesheni ya SGR jijini Dar es Salaam, Aprili 2024.

**Inatoka Uk. 01**

"Leo ni siku ya kihistoria kuelekea kilele cha miaka sitini ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, uzinduzi wa njia ya reli kutoka Dar es Salaam - Dodoma inaonesha thabiti hatua chache zilizobaki ili tuanze safari rasmi, jambo la furaha zaidi kundi la kwanza kuzindua safari hii ni viongozi wa Dini" alisema Waziri Mkuu.

Aidha, Waziri Mkuu aliongeza kuwa safari ya viongozi wa Dini kwa treni ya majaribio Dar es Salaam hadi Dodoma ni kuendeleza tunu ya Taifa ya Amani iliyopo nchini kutokana na watanzania wengi kuwa waumini na Imani za Dini mbalimbali.

"Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan anawaasa viongozi wa Dini kuendelea kuliombea Taifa kwani Taifa linajengwa kwa misingi imara ya Dini, Serikali inaheshimu Dini kwani ina mchango mkubwa kwa Taifa katika maendeleo" Amesema Mhe.Majaliwa.

Naibu Waziri wa Uchukuzi Mhe. David Kihenzile amewahakikishia watanzania kuwa ifikapo mwezi Julai 2024 treni za SGR zitaanza kusafirisha abiria rasmi kutoka Dar es Salaam hadi Dodoma.

Mkurugenzi Mkuu TRC Ndugu Masanja Kungu Kadogosa ameeleza kuwa katika kuadhimisha miaka 60 ya Muungano wa Tanzania miongoni mwa mafanikio ya Serikali ni ujenzi wa Reli ya kimkakati ya kimataifa ya SGR ambao unatekelezwa kwa gharama ya Dola za Kimarekani Bilioni 10.01 sawa na Shilingi za kitanzania trilioni 23.3 na utekelezaji wake uko katika hatua mbalimbali.

"Kazi ya majaribio inaendelea kufanyika kwa vichwa na mabehewa ya abiria ,tunasubiri Sana mabehewa ya mizigo kwani huko ndipo kwenye faida na fursa za uchumi zaidi" Amesema Ndugu Kadogosa.

"Tunamshukuru Mhe. Rais kwa hatua hii, kama viongozi wa Dini tunaendelea kuiombea nchi na Serikali kwa ujumla katika utekelezaji wa majukumu yake" Amesema Mchungaji wa Kanisa la Kiinjili la Kikutheri Tanzania (KKKT) Jimbo la Mashariki na Pwani Usharika wa Makongo George Fupe.

Shirika la Reli Tanzania linajiandaa kuanza kwa shughuli za uendeshaji treni za SGR na mpaka sasa tayari imepokea mabehewa 65 Kati 89 ya abiria na vichwa 9 kati ya 19 na seti moja kati ya 10 za treni ya kisasa (EMU).



# BUNGE LAPITISHA TRILIONI 1.511 KUENDELEZA MRADI WA SGR NCHINI

**Na Mwandishi wetu**

Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania limepitisha Trilioni 1.511 kuendeleza mradi wa ujenzi wa reli ya kiwango cha kimataifa – SGR kwa mwaka wa fedha 2024/25 ikiwa ni sehemu ya Shilingi Trilioni 2.7 ya bajeti ya Wizara ya Uchukuzi kwa mwaka 2024/25.

Waziri wa Uchukuzi Mhe. Prof. Makame Mbarawa ametaja vipaumbele vya Wizara katika Sekta ya reli ambavyo ni kuendeleza ujenzi wa reli ya kiwango cha kimataifa (Standard Gauge Railway - SGR) katika maeneo yaliyobaki pamoja na ununuzi wa vitendea kazi (vichwa na mabehewa) ambapo jumla ya Shilingi trilioni 1.511 zimetengwa, kufufua reli ya MGR kipande cha Kilosa – Kidatu Kilomita 108 ambapo kimetengwa kiasi cha Shilingi bilioni 1 na ukarabati wa reli iliyopo ya MGR ambapo Shilingi bilioni 312.03 zimetengwa.

Taarifa ya Mhe. Mbarawa imeeleza kuwa Shirika la Reli Tanzania linaendelea na mradi wa ujenzi wa reli ya kiwango cha kimataifa – SGR kwa ushoroba wa kati awamu zote mbili ambapo awamu ya kwanza ina jumla ya kilomita 1219 na awamu ya pili ina jumla ya kilomita 1590 na hivyo kuifanya reli mpya ya SGR inayojengwa kuwa na mtandao wa kilomita 2809 ambapo kipande cha kutoka Dar es Salaam hadi Dodoma kikiwa mbioni kuanza uendeshaji.

Aidha, Prof. Mbarawa amesema kuwa Sekta ya Uchukuzi imeendelea kutoa mchango mkubwa wa ukuaji uchumi kwa taifa kwa kuwa ni sekta wezeshi katika kuchagiza ukuaji wa sekta nyingine za madini, utalii, viwanda na biashara mathalani katika mwaka 2022 Sekta ya uchukuzi ilikua kwa asilimia 3.8 na kuchangia katika pato la Taifa kwa asilimia 6.7. Sekta ya Uchukuzi ni ya tatu katika kuchangia fedha za kigeni kupitia mauzo ya huduma ambapo katika kipindi cha miaka mitatu mchango wa sekta hii katika fedha za kigeni umeongezeka kwa kiasi kikubwa kutoka Dola za

Inaendelea Uk. 4

# BUNGE LAPITISHA TRILIONI 1.511 KUENDELEZA MRADI WA SGR NCHINI

Inatoka Uk. 3

kimarekani bilioni 1.6 mwaka 2022 hadi dola bilioni 2.4 mwaka 2024 sawa na ongezeko la asilimia 50.

"Katika kutekeleza maagizo ya Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Samia Suluhu Hassan ya kuanza uendeshaji wa huduma za treni katika reli ya SGR kipande cha Dar es Salaam hadi Dodoma, TRC inaendelea na mikakati ya kuhakikisha inaanza huduma mwezi Julai 2024" aliongeza Prof. Mbarawa

Prof. Mbarawa akijibu hoja wakati wa majumuisho amesema kuwa ili iweze kukidhi viwango bora na kuwepo kwa viwango bora, Serikali imeendelea kuweka mifumo mbalimbali ya kufuatilia miradi ya maendeleo ikiwemo kuweka kituo cha kufuatilia miradi na thamani ya uwekezaji katika miradi.

"Ninaamini mradi wetu wa SGR unatekelezwa kwa viwango vizuri sana, nchi mbalimbali zimekuja kujifunza ikiwemo Uganda, Ethiopia, DRC, Burundi na nchi nyingine wamekuja kujifunza" alisisitiza Prof. Mbarawa

Mkurugenzi Mkuu wa Shirika la Reli Tanzania Masanja Kadogosa amemshukuru Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Samia Suluhu Hassan kwa kuendelea kutenga fedha pamoja na Bunge kuidhinisha bajeti ya uboreshaji na ujenzi wa miundombinu mipya ya reli nchini.

Bajeti ya Wizara ya Uchukuzi pamoja na mambo mengine inatarajiwa kufanya mabadiliko makubwa ya usimamizi na uwezeshaji wa masuala ya miundombinu ya Uchukuzi nchini kwa njia ya Anga, Usafiri ardhini ukihusisha masafa marefu na mafupi, Usafiri kwa njia ya maji ukijumuisha ujenzi na ukamilishwaji wa vituo vya utafutaji na uokoaji majini, huduma za hali ya hewa, bandari na mitambo ya kufundishia vyuoni ambavyo vitachochea ukuaji wa uchumi katika maeneo mbalimbali.



Waziri wa Uchukuzi Mhe. Prof. Makame Mbarawa (kushoto) na Naibu Waziri wa Uchukuzi Mhe. David Kihenzile wakizungumza jambo wakati wa uwasilishaji Bajeti ya Wizara ya Uchukuzi kwa mwaka wa fedha 2024/25 Bungeni jijini Dodoma, hivi karibuni 2024.



Waziri wa Uchukuzi Mhe. Prof. Makame Mbarawa (kati), Naibu Waziri wa Uchukuzi Mhe. David Kihenzile (wa pili kushoto), kutoka kulia nyuma Katibu Mkuu Uchukuzi Prof. Godius Kahyarara, Naibu Katibu Mkuu Dkt. Ally Possi na Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi TRC Ally Karavina katika picha ya pamoja Bungeni jijini Dodoma, hivi karibuni 2024.



Baadhi ya Viongozi wa Wizara ya Uchukuzi na Taasisi zilizo chini ya Wizara ya Uchukuzi wakifuatilia majadiliano wakati wa uwasilishaji wa Bajeti ya Wizara ya Uchukuzi kwa mwaka wa fedha 2024/25 Bungeni jijini Dodoma, hivi karibuni 2024



Kaimu Mkurugenzi Mkuu wa Shirika la Reli Tanzania Bi. Amina Lumuli (wa kwanza kulia) akizungumza na baadhi ya Makatibu Wakuu wastaafu wa Wizara mbalimbali nchini ndani ya treni ya kisasa walipofanya ziara kukagua mradi wa ujenzi wa reli ya kiwango cha kimataifa - SGR kuanzia Dar es Salaam hadi Morogoro Aprili 13, 2024

# MAKATIBU WAKUU WASTAAFU WAIPONGEZA SERIKALI KUENDELEZA MRADI WA SGR

**Na Mwandishi wetu**

Naibu Katibu Mkuu Wizara ya Uchukuzi Dkt. Ally Possi akiambatana na Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi Shirika la Reli Tanzania – TRC Bwana Ally Karavina wameongoza Umoja wa Makatibu Wakuu Wastaafu Tanzania (UMWAWATA) katika ziara kukagua mradi wa ujenzi wa reli ya kiwango cha kimataifa – SGR kuanzia Dar es Salaam hadi Morogoro, Aprili 13, 2024.

Lengo la ziara ni kuwapatia elimu na uelewa Makatibu Wakuu wastaafu wakiwa ni sehemu ya washauri wa masuala mbalimbali katika shughuli za kiutendaji katika Serikali. Pia ziara hiyo ni sehemu ya muendelezo wa majaribio ya safari za treni kwaajili ya kukamilisha utayari wa kuanza kutoa huduma za usafiri wa treni katika reli ya kiwango cha kimataifa.

Naibu Katibu Mkuu Dkt. Possi amesema Wizara kupitia Shirika la Reli inaendelea na maandalizi kuhakikisha maagizo ya Mhe. Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan ya kuanza uendeshaji wa SGR ifikapo Julai yanafanikiwa kabla ya mwezi Julai.

"Sisi kama Wizara tumeanza kutekeleza maelekezo hayo na sisi tunataka kuanza mapema ifikapo mwezi Juni, lakini si kuanza tu kwa abiria tunaanza pia kuangalia utayari wa kubeba mizigo, kwasababu tunafahamu faida ya uwekezaji ambao Serikali imeweka" alisema Dkt. Possi

Mwenyekiti wa UMWAWATA Bwana Michael Mwanda amelishukuru Shirika la Reli Tanzania kwa kuuwezesha umoja huo kufanya ziara kuona maendeleo ya mradi wa SGR ambapo pamoja na shukurani wamepongeza Serikali inayoongozwa na Mhe. Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kuendeleza mazuri yaliyoachwa na viongozi waliotangulia.

Inaendelea Uk. 6

# MAKATIBU WAKUU WASTAAFU WAIPONGEZA SERIKALI KUENDELEZA MRADI WA SGR



Naibu Katibu Mkuu Wizara ya Uchukuzi Dkt. Ally Possi (kati) akiwa katika picha ya pamoja na Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi Shirika la Reli Tanzania - TRC Ally Karavina (wa saba kushoto), Kaimu Mkurugenzi Mkuu TRC Bi. Amina Lumuli (wa tano kushoto) na Makatibu Wakuu wastaafu wa Wizara mbalimbali nchini baada ya ziara kukagua mradi wa ujenzi wa reli ya kiwango cha kimataifa - SGR kwa kutumia treni ya kisasa kuanzia Dar es Salaam hadi Morogoro Aprili 13, 2024

Inatoka Uk. 5

"uwezo wa reli hii ni mkubwa sana katika kubeba mizigo na najua kabisa wenzetu nchi za jirani wanatusubiri kwa hamu tuweze kumaliza hii kazi, tumezungukwa na nchi nyingi sana ikiwemo Congo, Zambia, Rwanda, Burundi na Uganda" alisema Bwana Mwanda.

Kaimu Mkurugenzi Mkuu wa Shirika la Reli Tanzania Bi. Amina Lumuli alisema kuwa kwa sasa majaribio ya kuendesha treni kipande cha Dar es Salaam – Morogoro yanaendelea vizuri, hivyo kipande cha Morogoro - Makutupora ambacho ujenzi wake umefika zaidi ya 96% majaribio yake yanatarajiwa kuanza hivi karibuni, lengo likiwa ni kuhakikisha mwezi wa saba uendeshaji unaanza rasmi.

Shirika la Reli Tanzania tayari limepokea jumla ya mabehewa 65 ya abiria, vichwa tisa vya umeme na seti moja ya treni ya kisasa ya abiria inayotumia nishati ya umeme (EMU) kwaajili ya kuanza majaribio, pia watumishi zaidi ya 400 tayari wamepatiwa mafunzo ndani na nje ya nchi kwaajili ya kuhakikisha shughuli za uendeshaji zinafanywa na watanzania ili kutoa huduma kwa ufanisi.

# TRC YASHIRIKI MAONESHO YA MAADHIMISHO YA MIAKA 60 YA MUUNGANO




Afisa Uhusiano kutoka Shirika la Reli Tanzania - TRC Bwana Hassan Mbonde akiwaonesha mtandao wa reli nchini baadhi ya wananchi waliotembelea banda la TRC katika maonesho ya Maadhimisho ya Miaka 60 ya Muungano wa Tanganyika na Zanzibar yaliyofanyika uwanja wa Mnazi Mmoja jijini Dar es Salaam, Aprili 19 hadi 25, 2024.

**Na Mwandishi wetu.**

Shirika la Reli Tanzania - TRC limeshiriki maonesho ya Muungano katika kuadhimisha miaka 60 ya Muungano wa Jamhuri ya Tanzania yaliyofunguliwa na Makamu wa pili wa Rais Zanzibar Mhe. Ahmed Suleimani katika viwanja vya Mnazi Mmoja jijini Dar es Salaam, Aprili 2024.

Meneja Msaidizi wa kipande cha kwanza Mhandisi David Msusa amesema kuelekea miaka 60 ya Muungano wa Jamhuri ya Tanzania TRC imeweza kusimamia ujenzi wa mradi wa kimkakati wa ujenzi wa reli ya kiwango cha kimataifa - SGR ambao unatekelezwa na Serikali ya awamu ya sita kuanzia Dar es Salaam hadi Mwanza na Tabora hadi Kigoma.

"Kuelekea miaka 60 ya Muungano TRC inatarajia kuanza safari za treni za abiria mwezi Julai kutoka Dar es Salaam hadi Dodoma na maandalizi yamefanyika ya kutosha na vitendea kazi vimewasili na timu ya wataalamu inaendelea na majaribio ya safari za treni ya abiria kutoka Dar es salaam hadi Dodoma" ameongeza Msusa.

Pia Mhandisi Msusa ameongeza kuwa reli ya SGR inatumia mwendokasi wa kilomita 160 kwa saa na treni ya mizigo itakua na uwezo wa kubeba takribani tani elfu kumi kwa safari.

TRC inasimamia uendeshaji wa reli ya kati (MGR) na reli ya kiwango cha kimataifa (SGR) pamoja na miradi yote inayoendeshwa TRC ikiwemo ukarabati wa miundombinu ya reli.

# MATUKIO KATIKA PICHA



Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Kassim Majaliwa akiingia ndani ya kichwa cha treni ya kisasa kinachotumia nishati ya umeme kabla ya safari ya kwanza ya majaribio ya treni ya abiria kuanza kutoka Dar es Salaam hadi Dodoma, Aprili 2024.



Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Kassim Majaliwa akizungumza na Mkurugenzi Mkuu wa Shirika la reli Tanzania Ndugu Masanja Kadogosa ndani ya kichwa cha treni ya kisasa kinachotumia nishati ya umeme kabla ya safari ya kwanza ya majaribio ya treni ya abiria kuanza kutoka Dar es Salaam hadi Dodoma, Aprili 2024.



Waziri wa Uchukuzi Mhe. Prof. Makame Mbarawa (kushoto) akikabidhi sadaka kwa mlezi wa kituo cha watoto yatima cha Amani Foundation Bi. Zubeda Makame wakati wa iftari na Dua ya pamoja kumuombea Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan na kuanza kwa uendeshaji wa huduma za usafiri katika reli ya kiwango cha kimataifa - SGR jijini Dar es Salaam Aprili 2024.



Mkurugenzi Mkuu wa TRC Masanja Kadogosa (wa pili kulia) akitoa neno la shukurani mara baada ya iftar na dua ya pamoja kumuombea Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan na kuanza kwa uendeshaji wa huduma za usafiri katika reli ya kiwango cha kimataifa - SGR jijini Dar es Salaam Aprili 2024.



Muonekano wa sehemu ya mbele ya seti ya treni ya kisasa inayotumia nishati ya umeme EMU (Electric Multiple Unit) iliyowasili nchini Aprili 2024

# KAMATI YA BUNGE YA PIC YARIDHISHWA KUANZA SAFARI ZA SGR



Meneja Mradi Msaidizi wa Mradi wa ujenzi wa reli ya kiwango cha kimataifa - SGR Dar es Salaam - Morogoro Mhandisi David Msusa akiwaelezea wajumbe wa kamati ya Bunge ya Uwekezaji wa Mitaji ya Umma kuhusu chumba cha uongozaji wa treni katika jengo la SGR, jijini Dar es Salaam, hivi karibuni 2024.

**Na Mwandishi wetu**

Shirika la Reli Tanzania - TRC limepokea ugeni kutoka kamati ya kudumu ya Bunge ya Uwekezaji wa Mitaji ya Umma - PIC na kufanya ziara ya ukaguzi wa mradi wa ujenzi wa reli ya kiwango cha kimataifa - SGR kutoka Dar es Salaam hadi Morogoro hivi karibuni 2024.

Makamu Mwenyekiti wa kamati ya kudumu ya bunge Uwekezaji wa Mitaji ya Umma Mhe. Augustine Vuma alisema kwa niaba ya kamati kuwa wameridhishwa na viwango vizuri vya miundombinu ya ujenzi huo.

"Mradi umejengwa katika viwango vizuri na vinavyostahili na safari zitakapoanza zitapunguza abiria kukaa kwa muda mrefu wakiwa safarini" alisema Mhe. Vuma.

Aidha, Mhe. Vuma alisema utekelezaji wa mradi umetoa ajira ya moja kwa moja zaidi ya elfu 30 na ajira ambazo sio za moja kwa moja 150,000 na kuwezesha kipato cha zaidi ya bilioni 650.

"Gharama za usafirishaji wa mizigo zitapungua kwa asilimia 40, kwa jinsi tulivyoshuhudia maelekezo ya Mhe. Rais ya kwamba treni ianze uendeshaji Julai mwaka huu inaenda kukamilika" alieleza Mhe. Vuma


Mwenyekiti wa Bodi ya wakurugenzi ya TRC Prof. Ally Karavina ameeleza kuwa majaribio yanaendelea vizuri na asilimia kubwa ya mradi kwa kipande cha kwanza umekamilika.

"Tuwaondoe hofu watanzania kwamba mradi huu wa kimkakati utaleta tija ya kukuza maendeleo ya taifa letu" alisema Karavina.

Naye Mkurugenzi Mkuu kutoka TRC Ndugu Masanja Kadogosa ameishukuru Kamati ya PIC kwa kuridhika baada ya kukagua mradi kwa kutumia treni ya umeme ya SGR pamoja na kuona mifumo ya uendeshaji inavyofanya kazi kwa uhakika.

"Kitu kikubwa ni sisi kuendelea kuchapa kazi ili kuhakikisha kwamba mwezi Julai safari za kutoka Dar Es Salaam hadi Dodoma zinaanza" alisema Ndugu Kadogosa.

# MAPINDUZI MAKUBWA KATIKA SEKTA YA MIUNDOMBINU YA RELI NCHINI



Treni ya kisasa ya abiria ikiwa katika stesheni ya reli ya kiwango cha kimataifa - SGR mara baada ya kuwasili jijini Dodoma katika safari ya majaribio kutoka Dar es Salaam, Aprili 2024.

**Na Mwandishi wetu.**

Shirika la Reli Tanzania - TRC limefanya mkutano na wahariri pamoja na waandishi wa habari katika jengo la stesheni ya SGR lililopo jijini Dar es Salaam Machi 25, 2024.

Mkutano huo ambao ulilenga kuelezea mapinduzi yaliyofanywa na Serikali ya Jamuhuri ya muungano wa Tanzania katika sekta ya miundombinu ya reli Tanzania na katika miaka mitatu ya uongozi wa Rais. Dkt. Samia Suluhu Hassan.

Mkurugenzi Mkuu TRC Ndugu Masanja Kungu Kadogosa alieleza kuwa TRC inaendelea na ukarabati wa njia ya kati kupitia mradi wa 'Tanzania Intermodal and Rail Development Project - TIRP'.

“Mtandao wa reli umegawanyika katika kanda tatu, ambazo ni kanda ya Kati, ukanda wa Kusini na ukanda wa Kaskazini” alieleza Ndugu Kadogosa.

Vilevile Ndugu Kadogosa alisema kuwa TRC inaendelea na ujenzi wa reli ya kiwango cha kimataifa - SGR kwa awamu ya kwanza inayojumuisha ujenzi wa mtandao wa reli wenye jumla ya kilomita 1,219 kutoka Dar es Salaam - Mwanza.

“Ujenzi huu wa SGR utakua moja ya nyenzo kubwa katika sekta ya uchukuzi nchini” alieleza Ndugu Kadogosa.

Aidha, Ndugu Kadogosa alieleza kuwa Serikali imekuwa ikiweka msukumo wa kibajeti wa utengaji rasilimali fedha ili kuhakikisha ujenzi wa miundombinu ya reli unatekelezwa na kukamilika kwa wakati.

“Wakati Mhe. Rais anaingia madarakani, kwa upande wa reli alikuwa muwazi na kuahidi kumalizia kipande alichokikuta na kuendeleza vipande vingine” aliongezea Ndugu Kadogosa.

**Inaendelea Uk. 11**

# MAPINDUZI MAKUBWA KATIKA SEKTA YA MIUNDOMBINU YA RELI NCHINI






Muonekano wa jengo la stesheni ya SGR jijini Dar es Salaam lenye uwezo wa kuhudumia abiria 1500 kwa siku likiwa imekamilika Aprili, 2024



Muonekano wa jengo la stesheni ya SGR jijini Dodoma lenye uwezo wa kuhudumia abiria 1500 kwa siku likiwa katika hatua za mwisho za ujenzi Aprili, 2024.

**Inatoka Uk. 10**

-

Mkuu wa Kitengo cha Uhusiano kutoka TRC Bi. Jamila Mbarouk alitoa shukurani kwa wahariri na waandishi wa habari kwa kufikisha taarifa sahihi za miradi inayotekelezwa na TRC pamoja na maendeleo yanayofanywa na serikali ya awamu ya sita katika sekta ya reli.

“Watu wa tasnia ya habari ni mabalozi sahihi wa kufikisha taarifa kwa umma, TRC inathamini mchango wenu kwa kuweza kuhakikisha taarifa zinafika wakati sahihi kwa umma kwa kudumisha maendeleo ya taifa letu” alisema Bi. Jamila.

Mhariri Mkuu wa Africa Media Group Limited Bi. Esther Zelamula ambaye amewawakilisha wahariri wa vyombo mbalimbali vya habari nchini alisema kuwa jukumu la wanahabari ni kushiriki kikamilifu katika kutangaza mazuri yanayofanywa na Serikali pamoja na Shirika la reli.

“Vyombo vya habari ni mhimili wa nne wa Dola, hivyo vina umuhimu mkubwa kwa umma na hatuna budi kuwa na uzalendo” alisema Bi. Esther.

Hata hivyo TRC inaendelea na ununuzi wa vitendea kazi kwaajili ya uendeshaji na ukarabati wa reli ambavyo umegawanyika katika makundi matano ikiwemo ununuzi wa vichwa vya umeme (Electric Locomotive) 19, Seti za treni ya umeme (Electric Multiple Unit) 10, mabehewa ya abiria 59, mabehewa ya mizigo 1,430 pamoja na mashine na mitambo 24 ya matengenezo ya njia ya SGR.




BODI YA WAHARIRI
MHARIRI MKUU | Jamila Mbarouk, MHARIRI MSAIDIZI/MSANIFU | Sami Omary
HABARI | Hemed Mohamed, Mariam Katunge MAKALA | Aziza Charles, Amina Juma, Athumani Iddy
PICHA | Hassan Mbonde, Augustino Bulegea